JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

# MAMLAKA YA UDHIBITI WA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO

## MWONGOZO WA BIASHARA YA MAZAO KATIKA MIPAKA

## (KASUMULU BUSINESS MODEL)

**Mfumo wa Kurasimisha Biashara ya Mipakani kwa Nafaka na Mazao Mchanganyiko**

**Aprili, 2026**


*Jengo la Kahawa Plaza, Mtaa wa Njedengwa, S.L.P2780, Dodoma-Tanzania.*
*Simu:+255262310225, Baruapepe:info@copra.go.tz.*

## 1.0 Usuli

Biashara ya mazao ya nafaka na mazao mchanganyiko katika mpaka wa Kasumulu, Wilaya ya Kyela, Mkoa wa Mbeya, imekuwa na mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa wananchi wa maeneo ya mipakani pamoja na kuimarisha biashara ya kikanda hususan kati ya Tanzania na nchi jirani ya Malawi. Pamoja na umuhimu huo, biashara hii imekuwa ikifanyika kwa muda mrefu bila mfumo rasmi unaoweza kuitambua, kuifuatilia na kuiwezesha kuchangia kikamilifu katika takwimu na mapato ya Serikali.

Kutokana na hali hiyo, Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) ilichukua hatua za kurasimisha biashara ya mazao katika eneo hilo kwa kuanzisha mfumo wa stakabadhi za ghala kupitia ukusanyaji uliokuwa ukifanyika chini ya Chama Kikuu cha KYECU. Hata hivyo, kutokana na uhalisia wa biashara ya mpakani Kasumulu ambapo sehemu kubwa ya mazao huingia kutoka nchi jirani hususan Malawi na siyo uzalishaji wa ndani wafanyabiashara waliona kuwa mfumo huo hauendani na mazingira ya biashara yao. Hali hii ilisababisha kujitokeza kwa changamoto mbalimbali ikiwemo kupungua kwa kasi ya biashara, kuongezeka kwa gharama za uendeshaji na hatimaye kuathiri shughuli za wafanyabiashara waliokuwa wakitegemea soko hilo.

Katika kukabiliana na hali hiyo, wafanyabiashara kupitia Ukanda wa Ukuaji wa Kilimo Tanzania (AGCOT) waliwasilisha malalamiko yao Serikalini kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, wakieleza athari za kusitishwa kwa biashara pamoja na kuomba kuwepo kwa utaratibu rasmi, rafiki na unaotambulika kisheria utakaoendelea kuruhusu biashara kufanyika kwa ufanisi bila kuathiri maslahi ya Taifa.

Kufuatia malalamiko hayo, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda na Biashara iliandaa ziara maalum wilayani Kyela iliyohusisha viongozi na wataalamu kutoka taasisi mbalimbali ikiwemo COPRA, TMX, WRRB, TCDC, TRA pamoja na Wizara husika. Ziara hiyo ilijumuisha kikao cha pamoja na wadau kilichofanyika tarehe 31/03/2026, ambapo changamoto za biashara ya mazao katika mpaka wa Kasumulu zilijadiliwa kwa kina na kupendekezwa hatua za kuanzisha mfumo rasmi wa kusimamia biashara hiyo.

Moja ya maazimio muhimu ya kikao hicho ilikuwa ni kuundwa kwa kamati maalum chini ya uongozi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya yenye jukumu la kuandaa mfumo wa kurasimisha biashara ya mazao katika soko la Kasumulu. Kamati hiyo iliundwa na wataalamu kutoka taasisi mbalimbali za Serikali ikiwemo COPRA, TMX, WRRB, TCDC, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Viwanda na Biashara, Serikali ya Mkoa, Wawakilishi wa wafanyabiashara kutoka eneo la Kasumulu na mwakilishi

kutoka TNCC. Orodha kamili ya wajumbe wa kamati hiyo imeainishwa katika Jedwali Na. 2 mwishoni mwa mwongozo huu.

Kupitia mchakato huo shirikishi, kamati iliandaa mfumo maalum unaojulikana kama *Kasumulu Business Model*, unaolenga kurasimisha biashara ya mazao ya mpakani kwa kuzingatia uhalisia wa biashara inayofanyika katika eneo hilo, huku ukihakikisha uwepo wa takwimu sahihi, ufuatiliaji wa mizigo na ongezeko la mapato ya Serikali.

## 2.0 Utangulizi

Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) ina jukumu la kuhakikisha biashara ya nafaka na mazao mchanganyiko nchini inafanyika kwa utaratibu, uwazi, uhalisia wa takwimu na kwa kuzingatia maslahi ya Taifa. Katika kutekeleza jukumu hilo, COPRA imeendelea kuanzisha na kusimamia mifumo mbalimbali ya kurasimisha biashara ikiwemo mfumo wa stakabadhi za ghala na minada ya kidigitali, kilimo cha mkataba (contract farming), mfumo wa wakusanya mazao (aggregators), mauzo ya moja kwa moja (direct sales) pamoja na ujenzi wa vituo vya kukusanyia mazao.

Hata hivyo, uzoefu umeonesha kuwa hakuna mfumo mmoja unaoweza kutumika kwa ufanisi katika maeneo yote ya biashara. Mazingira ya uzalishaji, aina ya zao, muundo wa biashara, aina ya wahusika, miundombinu na tabia ya soko hutofautiana kutoka eneo moja hadi jingine. Kwa mfano, maeneo ambayo vyama vya ushirika vimeimarika, mfumo wa stakabadhi za ghala na minada ya kidigitali umeweza kufanya kazi vizuri. Lakini kwa maeneo ya mipakani yenye biashara ya haraka, inayofanywa na wafanyabiashara binafsi, transit trade na mauzo ya moja kwa moja kwa wanunuzi wa nje, mifumo hiyo imekuwa na changamoto kubwa.

Maeneo ya mpaka wa Kasumulu ni mifano hai ya mazingira hayo. Kwa muda mrefu maeneo haya yamekuwa kitovu cha biashara ya mazao kutoka nje ya nchi, ambapo mazao kama soya, ufuta, mbaazi, maharage na mazao mengine huuzwa kwa ajili ya matumizi ya ndani au kusafirishwa kwenda masoko mengine ya ndani na nje ya Tanzania.

Kwa kuwa sehemu kubwa ya mazao hayo yanayotoka katika eneo tajwa husafirishwa nje ya nchi kupitia mipaka mbali mbali ya Tanzania na hasa bandari ya Dar es salaam, hupata changamoto katika rekodi za taarifa za uzalishaji na hivyo Taifa limekuwa likikosa takwimu sahihi za uzalishaji, biashara, mauzo ya nje na mchango wa mazao husika katika uchumi. Hali hii imekuwa ikiathiri upangaji wa sera, uhalisia wa takwimu za uzalishaji, makadirio ya mahitaji ya soko, pamoja na mipango ya kuongeza thamani kwa mazao.

Kutokana na changamoto hiyo, inapendekezwa kuanzishwa kwa "Kasumulu Border Business Model", mfumo maalum wa biashara ya mipakani unaotambua uhalisia wa biashara inayofanyika katika maeneo hayo, lakini wakati huo huo ukiirasimisha, kuipa ufuatiliaji wa kidigitali, kuongeza mapato ya Serikali na kuhakikisha mazao yanayotoka nje ya nchi hayachanganywi na takwimu za mazao ya ndani.

## 3.0 Tatizo Linalolengwa na Mfumo

Mfumo uliopo sasa una changamoto zifuatazo:

i. Soko la Kasumulu/Tunduma (na mipaka mingine) hutumika kuuza bidhaa zinazozalishwa katika maeneo ya mpakani pande za ndani na nje ya Tanzania.
ii. Takwimu za uzalishaji katika maeneo haya na mauzo ya nje zimekuwa si sahihi.
iii. Mfumo wa stakabadhi za ghala haujafanya kazi vizuri katika maeneo haya kwa kuwa wahusika wakuu ni wafanyabiashara wa mpakani na si wakulima wala vyama vya ushirika.
iv. Serikali imekuwa ikikosa sehemu ya mapato kutokana na biashara kubwa inayofanyika katika maeneo haya.
v. Hakuna mfumo rasmi wa kumtambua muingizaji, mnunuzi, kiasi, ubora, asili ya mzigo na mwisho wa mzigo kwenda.
vi. Biashara nyingi zinafanyika kwa njia zisizo rasmi hivyo kuongeza hatari ya utoroshaji, ukwepaji wa tozo na upotevu wa taarifa muhimu.
vii. Mfumo wa biashara wa sasa unahatarisha wakazi wa maeneo haya kufanya biashara na hivyo kushindwa kumudu maisha.

## 4.0 Dira ya Mfumo

Kuanzisha mfumo rasmi, rahisi, wa kidigitali na unaokubalika kwa wadau wote wa biashara ya mpakani katika Kasumulu na Tunduma (na maeneo mengine), wenye;

i. Kurasimisha biashara ya mazao ya mpakani;
ii. Kuhifadhi uhalisia wa takwimu za uzalishaji na biashara;
iii. Kuongeza mapato ya Serikali;
iv. Kupunguza biashara holela na utoroshaji;
v. Kuwezesha ufuatiliaji wa mzigo kutoka unapoingia mpaka unapoondoka;
vi. Kulinda mifumo mingine ya biashara inayotumika nchini;
vii. Kutoa mazingira rafiki kwa wafanyabiashara wa mpakani kuendelea na biashara zao bila kuzuiwa.

## 5.0 Malengo ya Mfumo

### 5.1 Lengo Kuu

Kurasimisha biashara ya nafaka na mazao mchanganyiko inayofanyika katika maeneo ya mipaka ya Kasumulu/Tunduma (na maeneo mengine) kwa kutumia mfumo maalum wa ukaguzi, usajili, ufuatiliaji wa kidigitali.

### 5.2 Malengo Mahususi

i. Kutambua na kusajili wafanyabiashara wote wa mipakani na wanunuzi wao.
ii. Kuboresha mazingira ya uzalishaji na tija ya mazao husika.
iii. Kurekodi kiasi halisi cha mazao yanayoingia nchini kupitia mipaka hiyo.
iv. Kutofautisha mazao kwa ajili ya matumizi ya ndani na mazao yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi (transit goods)
v. Kukusanya mapato ya maendeleo ya zao na tozo nyingine za Serikali.
vi. Kuhakikisha mazao yote yanayoingia yana ubora unaokubalika.
vii. Kuweka mfumo wa kidigitali wa kufuatilia mzigo hadi unapofika kwa mlaji wa mwisho.
viii. Kutoa takwimu sahihi kwa ajili ya kupanga sera na maamuzi ya Serikali.

## 5.0 Muundo wa Biashara

Mfumo unapendekezwa kujengwa katika nguzo sita kuu:

1. Usajili wa Wafanyabiashara wa Mipakani;
2. Vituo vya Mpakani vya COPRA;
3. Ukaguzi na Uthibitishaji wa Mazao;
4. Mfumo wa Kidigitali wa COPRA MIS;
5. Kibali cha kusafirisha Mzigo;
6. Mfumo wa Mapato na Ushirikiano wa Taasisi.

## 6.0 Nguzo ya Kwanza: Usajili wa Wafanyabiashara wa Mipakani

COPRA itaanzisha utaratibu maalum wa usajili kwa wafanyabiashara wote wanaofanya biashara ya mazao katika maeneo ya Kasumulu, Tunduma na mengineyo.

### 6.1 Wadau watakaosajiliwa

- Wauzaji wa mipakani;
- Kampuni za usafirishaji;
- Wanunuzi wa mazao kutoka maeneo ya mipaka.

- Mawakala wa usafirishaji walioko mpakani
- Wachukuzi wa mazao walioko mpakani (Makuli)
- Maeneo ya kupakua na kupakia mazao

**6.2 Taarifa Zitakazokusanywa**

- Leseni ya biashara
- Cheti cha usajili wa Kampuni/Kitambulisho cha NIDA;
- Namba ya usajili wa biashara/TIN;
- Aina ya mazao anayofanya biashara;
- Kiwango cha biashara kwa mwezi/mwaka;
- Masoko anayouza;
- Orodha ya wanunuzi wake wa kawaida;
- Maghala au maeneo ya kuhifadhi anayotumia.

**6.3 Faida ya Usajili**

- Serikali itawajua wahusika wote;
- Itarahisisha ufuatiliaji wa mizigo;
- Itasaidia kupunguza biashara haramu;
- Itarahisisha utoaji wa vibali na huduma;
- Wafanyabiashara watapata utambulisho rasmi na kuaminika.

Inapendekezwa kila muuzaji wa soko hilo apewe Border Trader Registration Number (BTRN) ambayo itatumika katika miamala yote.

**7.0 Nguzo ya Pili: Kuanzishwa kwa Vituo vya COPRA Mipakani**

COPRA itaanzisha kituo rasmi katika mpaka wa Kasumulu, Tunduma na maeneo mengineyo. Kituo hiko Kitakuwa ndiyo sehemu rasmi ya kupokea taarifa za mzigo, kukagua mazao, kupima na kuthibitisha kiasi cha mzigo na kuingiza taarifa kwenye mfumo wa COPRA MIS.

Ili kuimarisha utendaji, kwa upande wa Kasumuiu, vituo viwili vitaanzishwa katika mpaka; kimoja kitawekwa ndani ya jengo la forodha, na kingine nje ya jengo hilo kwa ajili ya kusimamia mchakato wa biashara baada ya kukamilika kwa taratibu zote za forodha.

## 8.0 Nguzo ya Tatu: Ukaguzi na Uthibitishaji wa Mazao

Mazao yote yanayoingia kupitia mipaka hiyo yatapitia ukaguzi kabla ya kupewa ruhusa ya kuendelea. Ukaguzi utalenga hasa; Magonjwa ya Mimea, Unyevu, Uwepo wa uchafu, Uharibifu wa punje, Mchanganyiko wa aina, Uzito halisi wa mzigo, Ufungashaji na Uhalali wa nyaraka za mzigo.

### 8.1 Uainishaji wa Mzigo

Baada ya ukaguzi mzigo utapewa kibali cha kusafirishia mzigo ambacho kitawezesha mzigo kusafirishwa hadi kufika kwenye mpaka wa kutokea. Kibali hiki kitatumika wakati wa ukaguzi katika vituo na pia kutumika wakati wa kutoa vibali vya kusafirisha mazao nje ya nchi.

## 9.0 Nguzo ya Nne: Mfumo wa Kidigitali wa COPRA MIS

Mfumo wa COPRA MIS utaboreshwa ili kuwa na "Border Trade Module" maalum kwa Kasumulu.

### 9.1 Taarifa Zitakazoingizwa Kwenye Mfumo

- Jina la mfanyabiashara;
- BTRN;
- Aina ya zao;
- Kiasi cha mzigo;
- Nchi ya asili ya zao;
- Mahali mzigo unapoenda;
- Jina la mnunuzi;
- Namba ya gari;
- Tarehe na muda wa kuingia;
- Ubora wa zao;
- Kiasi cha tozo kinachotakiwa kulipwa.

### 9.2 Mfumo Utakavyofanya Kazi

1. Mfanyabiashara anawasilisha mzigo kituoni;
2. Afisa wa COPRA atakagua mzigo;
3. Afisa anaingiza taarifa kwenye COPRA MIS;
4. Mfumo unatengeneza control number moja kwa moja;
5. Mfanyabiashara analipa kupitia benki au simu;
6. Mfumo unathibitisha malipo;
7. Kibali cha kusafirisha mzigo kitazalishwa;
8. Taarifa za mzigo zinaendelea kufuatiliwa hadi mwisho.

### 9.3 Taarifa Zitakazotolewa na Mfumo

Mfumo utaweza kutoa taarifa za:

- Kiasi cha mazao yaliyoingia kwa siku, mwezi na mwaka;
- Mahali mazao yalipotoka;
- Kiasi kilichouzwa ndani na nje;
- Mapato yaliyokusanywa;
- Wafanyabiashara wakubwa;
- Mwelekeo wa biashara kwa kila zao.

## 10.0 Nguzo ya Tano: Kibali cha Kusafirisha Mzigo

Baada ya mfanyabiashara kukamilisha ukaguzi na malipo, atapewa kibali cha kusafirisha mzigo. Kibali hiki ni hati au *electronic movement permit* yenye QR Code au serial number inayothibitisha kuwa:

- Mzigo umekaguliwa;
- Mzigo umelipiwa;
- Serikali inautambua;
- Mzigo unaruhusiwa kuendelea na safari.

Muda wa kibali kutumika utakauwa siku kumi na nne (14) toka siku ya kutolewa kwake. Mzigo utatakiwa kuwa umefika katika eneo la mwisho kabla ya siku 14 toka kutolewa kwa kibali na baada ya mnunuzi kufikisha mzigo katika eneo unakokwenda atatakiwa kuitaarifu Mamlaka na kibali kitafutwa. Iwapo zitapita siku 14 bila taarifa yoyote kuhusu mzigo kufika, kibali kitafutwa na mpokeaji wa mzigo atafuatiliwa na Mamlaka ili kueleza sababu za kutokutoa taarifa.

Na iwapo sababu za kuchelewa kutoa taarifa hazitakuwa za msingi, basi hatua za adhabu kufuatia **Mwongozo wa Biashara kwa mazao ya Ufuta, Choroko, Dengu, Mbaazi, Soya, Kunde na Njugumawe toleo la 4 – 2026** zitachukuliwa.

### 10.1 Taarifa Zitakazokuwa Kwenye Kibali cha kusafirisha mzigo

- Namba ya kibali;
- Jina la mfanyabiashara;
- Aina ya zao;
- Kiasi;
- Daraja la ubora;
- Chanzo cha zao;
- Mnunuzi;

- Mahali mzigo unapopelekwa;
- Namba ya gari;
- Tarehe ya kutoka Kibali
- Tarehe ya kuisha kwa kibali.

### 10.2 Matumizi ya Kibali

Kibali cha kusafirisha mzigo kitatakiwa kuoneshwa:

- Katika vituo vya ukaguzi barabarani;
- Katika maghala;
- Katika bandari au mipaka mingine;
- Kabla ya vibali vya kusafirisha mazao (export permit) au vibali vingine kutolewa.

**Ikumbukwe, bila kibali cha kusafirisha mzigo, mzigo hautatambuliwa rasmi.**

## 11.0 Nguzo ya Sita: Mfumo wa Tozo na Mapato

### 11.1 Tozo

Kwa kila kilo ya mazao yatakayopitia mfumo huu, serikali itakusanya kiasi kisichozidi shilingi 40 + 3% kwa kilo.

### 11.2 Mgawanyo wa tozo

| **Lengo la Tozo** | **Kiasi** |
|---|---|
| Maendeleo ya Zao | 30 |
| Wilaya | 05 |
| Mkoa | 05 |
| CESS | 3% |
| **Jumla** | **40 + 3%** |

Mapato yatakayokusanywa yagawanywe kama ifuatavyo:

- COPRA – kwa ajili ya kuhakikisha uwepo wa kituo cha ukaguzi, usimamizi wa mfumo, takwimu, na kuendeleza mazao;
- Halmashauri (kupitia CESS) – Usimamizi wa biashara, ukaguzi katika mageti;
- Wilaya na Mkoa – Kwa ajili ya Ulinzi na uwekaji wa miundombinu.

## 12.0 Wadau Muhimu na Majukumu Yao

| Taasisi | Jukumu |
|---|---|
| COPRA | Kuweka kituo cha ukaguzi, kusimamia mfumo, usajili, ukaguzi, takwimu na Exit Seal |
| TPHPA | Kuhakiki usafi na afya ya mimea katika kituo cha ukaguzi cha COPRA |
| Halmashauri | Kusaidia utekelezaji wa Mfumo na kusimamia mageti. |
| Wilaya na Mikoa | Kuweka ulinzi na miundombinu ya masoko |
| Wafanyabiashara | Kusajiliwa, kutoa taarifa sahihi na kulipa tozo |
| TNCC | Uthibitishaji wa wafanyabiashara wa mipakani |

## 13.0 Hatari Zinazoweza Kujitokeza na Namna ya Kuzidhibiti

| Hatari | Njia ya Kudhibiti |
|---|---|
| Wafanyabiashara kukwepa mfumo | - Kufanya usajili wa wahusika wote katika mfumo pamoja na vituo vya kupakia na kupakua<br>- Kufanya ukaguzi wa barabarani. |
| Mazao kutoka katika maeneo mengine kuuzwa kupitia soko la kasumulu | - Kuweka viwango linganishi vya tozo<br>- Kutambuwa wadau wote wanaohusika na soko la kusumulu kupitia usajili<br>- Wadau kusajiliwa baada ya kutambuliwa na Chama cha wafanyabiashara |
| Mzigo kubadilishwa njiani | - Kutumia QR Code katika kibali kutambua aina ya mzigo<br>- Kutambulisha msafirishaji na nambari ya gari inayosafirisha |
| Migongano kati ya taasisi | - Kuandaa mwongozo wa pamoja wa utekelezaji |

## 14.0 Mfumo wa Utawala (Governance), Udhibiti wa Hatari na Utekelezaji wa Sheria

Ili kuhakikisha kuwa mfumo wa biashara katika mpaka wa Kasumulu unafanya kazi kwa ufanisi na unadhibiti hatari zote zinazoweza kujitokeza, ni muhimu kuweka mfumo madhubuti wa utawala (governance framework) unaojumuisha sheria, kanuni, ufuatiliaji na adhabu.

### 14.1 Kanuni za Uendeshaji wa Biashara ya Mpakani

1. Biashara yote ya mazao kupitia mipaka ya Kasumulu kwa utaratibu ulioainishwa katika kipengele 9.2.
2. Usajili wa wafanyabiashara, wachukuzi na maeneo ya kupakua na kupakia mizigo utafanywa baada ya mhusika kutambuliwa na uongozi wa TNCC -Tawi la Kasumulu.
3. Kila mzigo lazima usajiliwe, ukaguliwe na upate kibali kabla ya kuendelea na safari.
4. Hakuna mzigo utakaoruhusiwa kusafirishwa bila kuwa kwenye mfumo wa COPRAMISS.
5. Wafanyabiashara wote lazima wawe wamesajiliwa na kuwa na BTRN hai.

### 14.2 Udhibiti wa Muda wa Biashara

Ili kupunguza mianya ya utoroshaji wa mazao, inapendekezwa kuweka muda rasmi wa biashara kama ifuatavyo:

- Biashara ya mazao mpakani ifanyike kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni (06:00 – 18:00) au muda wowote ambapo shughuli za forodha zitakuwa zikiendelea.
- Mizigo yote itakayokutwa njiani bila kibali ndani ya muda usioruhusiwa utakuwa sio halali.
- Kwa mizigo maalum (mfano export ya dharura), kibali maalum cha maandishi kutoka COPRA kitahitajika.

### 14.3 Udhibiti wa Njia Zisizo Rasmi (Panya Routes)

1. Kuimarisha doria za pamoja kati ya:
    - COPRA
    - Kikosi kazi cha mapato ya Halmashauri
    - Forodha (TRA)
    - TNCC
2. Kuweka vituo vya ukaguzi (checkpoints) kwenye maeneo hatarishi.
3. Kushirikisha jamii ya mipakani kutoa taarifa za utoroshaji.

### 14.4 Mfumo wa Adhabu na Faini (Penalties)

Iwapo kutakuwa na mazao yoyote yatakayouzwa kupitia eneo hili pasipo kufuata utaratibu uliowekwa katika Mwongozo huu yatahesabiwa kuuzwa nje ya Kasumulu Model na hivyo taratibu zilizowekwa katika **Mwongozo wa Biashara kwa mazao ya Ufuta, Choroko, Dengu, Mbaazi, Soya, Kunde na Njugumawe toleo la 4 – 2026** utafuatwa. Pia kwa makosa mengine ya kukiuka biashara kama ilivyowekwa na Mamlaka yataadhibiwa kufuata sheria mbali mbali za nchi ikiwemo Sheria ya Usalama wa Chakula Sura 249.

## 15.0 Faida za Mfumo kwa Taifa

Mfumo huu utawezesha:

i. Kupata takwimu sahihi za uzalishaji wa ndani.
ii. Kuongeza uzalishaji wa mazao husika.
iii. Kutenganisha mazao ya transit na mazao ya Tanzania.
iv. Kuongeza mapato ya Serikali.
v. Kupunguza biashara holela na utoroshaji.
vi. Kuwezesha wafanyabiashara kufanya biashara zao kwa utaratibu.
vii. Kulinda ushindani wa mazao ya ndani.
viii. Kuifanya Tanzania kuwa kitovu rasmi cha biashara ya mazao ya ukanda wa Kusini mwa Afrika.
ix. Kuongeza uwezo wa Serikali kupanga sera sahihi za mazao kama soya, ufuta, mbaazi na maharage.
x. Kuwezesha COPRA kuwa na database ya kweli ya biashara ya mpakani.
xi. Kuchochea uzalishaji wa mazao.

## 16.0 Hitimisho

Kasumulu ni eneo la kimkakati katika biashara ya mazao ya ukanda wa Kusini mwa Afrika. Kwa miaka mingi biashara inayofanyika katika maeneo hayo imekuwa na mchango mkubwa kwa wananchi na uchumi wa nchi, lakini imeendelea kufanyika bila mfumo rasmi unaoweza kuitambua, kuifuatilia na kuifanya ichangie kikamilifu katika takwimu na mapato ya Taifa.


Mfumo wa Kasumulu Border Business Model unapendekezwa kama suluhisho la kitaifa litakalowezesha Serikali kurasimisha biashara hiyo. Mfumo huu unatambua uhalisia wa biashara ya mpakani, unatoa nafasi kwa wafanyabiashara kuendelea na shughuli zao, lakini wakati huo huo unalinda maslahi ya Taifa kwa kuhakikisha kuwa kila mzigo unatambulika, unakaguliwa, unalipiwa na unafuatiliwa.

Kwa utekelezaji sahihi, mfumo huu utaifanya Tanzania kuwa kitovu rasmi cha biashara ya mazao ya mpakani katika ukanda wa SADC na COMESA, huku ukiweka

msingi wa takwimu sahihi, mapato zaidi na maendeleo endelevu ya sekta ya nafaka na mazao mchanganyiko.

Irene M. Mlola
Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka
Na Mazao Mchanganyiko (COPRA)

**Jedwali namba 1: Mchoro wa Mfumo wa Biashara Kasumulu**



**Jedwali namba 2: Timu ya Wataalamu Waliondaa Mwongozo wa Biashara mpaka wa Kasumulu**

| Na | Jina | Nafasi/Cheo | Taasisi |
|---|---|---|---|
| 1. | Said Madito | Mwenyekiti | RS- Mbeya |
| 2. | Abdallah Hamad | Katibu | AGCOT |
| 3. | Kamwesige M Mtembei | Mjumbe | COPRA |
| 4. | Samwel O Msuya | Mjumbe | COPRA |
| 5. | Emmanuel Mwanga | Mjumbe | COPRA |
| 6. | Petro Mabagala | Mjumbe | COPRA |
| 7. | Sebastiana Mwapinga | Mjumbe | RS- Mbeya |
| 8. | Anna Mwambene | Mjumbe | RS- Mbeya |
| 9. | Benard Libata | Mjumbe | RS- Mbeya |
| 10. | Kenneth Milano | Mjumbe | Kyela DC |
| 11. | Chresenga Mwimbwa | Mjumbe | Wizara ya Viwanda na Biashara |
| 12. | Emmanuel Mahinya | Mjumbe | Wizara ya Viwanda na Biashara |
| 13. | Khalid Mgaramo | Mjumbe | AGCOT |
| 14. | Prudence Lugendo | Mjumbe | AGCOT |
| 15. | Miriam Solomon | Mjumbe | AGCOT |
| 16. | Tulllah Mloge | Mjumbe | AGCOT |
| 17. | Mohamed Issa | Mjumbe | TRA |
| 18. | Novatus Kinano | Mjumbe | JWT |
| 19. | Mtatiro Kehengu | Mjumbe | Kyela DC |
| 20. | Denis Mrema | Mjumbe | Wizara ya Kilimo |
| 21. | Josephat Mwakalinga | Mjumbe | TNCC |
| 22. | Thobias Mwakyambo | Mjumbe | TNCC |
| 23. | Ayubu Mwakabanga | Mjumbe | TNCC |
| 24. | Erick Sichonga | Mjumbe | TNCC |